TANZANIA ASSEMBLIES OF GOD

TAMKO LA KUJIWEKA WAKFU KWA AJILI YA MIAKA 13 YA MOTO WA UAMSHO

(THE SEASON OF REVIVAL FIRE)

2020-2033

Kwa kuwa **TUNAAMINI** kuwa huu ni wakati wa uamsho, yaani kurudiwa kwa Pentekoste ndani ya Kanisa **(Matendo 2:1-4; 4:31)**; kwa kuwa **TUNAAMINI** juu ya yale yaliyotokea katika huduma ya Bwana wetu Yesu Kristo na katika kanisa la Matendo ya Mitume **(Matendo 10:38-40)** na ya kuwa tukiomba na kuvuviwa matendo hayo yaweza kutokea leo **(Yohana 14:12)**; kwa kuwa **TUNAAMINI** kuwa tamko la Halmashauri Kuu ya TAG lililopitishwa na Baraza la Waangalizi na kisha kuthibitishwa na Baraza Kuu kupitia konferensi za majimbo yote sabini na moja (71), kwamba miaka hii kumi na tatu (13) ya 2020-2033 na kuendelea, kuwa ni miaka ya moto wa uamsho ya kumtaka Bwana na **NGUVU ZAKE.** Kwa kuwa **TUNAAMINI** kuwa tumeisikia vema sauti ya Roho Mtakatifu ikiongea na mioyo yetu kama kanisa la nchi lenye maono makubwa, Sisi kanisa la ''Tanzania Assemblies of God'', tunatamka tamko la kujiweka **WAKFU** kwa Bwana na **UWEZA** wa **NGUVU ZAKE** kama ifuatavyo:

TUNAJIWEKA WAKFU kufunga na kuomba, kuimarisha ushirika na umoja wa kanisa na kuendelea kuhubiri mahubiri ya Kipentekoste tukitazama umwagiko wa Roho Mtakatifu katika nchi yote ya Tanzania na nje ya mipaka yake. Tukiomba sawasawa na **Mambo ya Nyakati wa pili 7:14 na Habakuki 3:2**; kwa ajili ya uamsho mkuu Tanzania unaoambatana na Nguvu za Kipentekoste, na udhihirisho na utendaji kazi wa Roho Mtakatifu kwa kiwango cha juu katika kanisa lake **(Matendo 1:8).**

TUNAJIWEKA WAKFU SISI WENYEWE kwa makusudi kabisa kutimiza **AGIZO KUU** ambalo linatutuma kuhubiri habari njema (Yesu anaokoa, Yesu anaponya, Yesu anajaza Roho Mtakatifu na Yesu anarudi tena) ulimwenguni kote na kwa kila kiumbe kwa kutumia mbinu mbalimbali **(Mathayo 28:19)** Tunaunganisha nguvu zetu katika taifa zima kama kanisa, pamojana washirika wenza ndani na nje ya nchi, wataosimama katika kuwasha moto wa Roho Mtakatifu na hivyo kumletea Mungu mavuno makubwa.

TUNAWAITA WATUMISHI NA WASHIRIKA WOTE wa TAG kujitoa dhabihu na kuonesha uzima mpya, nguvu mpya na uhai mpya kwa maombi, mifungo na mikesha **(Waefeso 6:18; Matendo 2:17-18)** kujenga ushirika na umoja wa kanisa; malezi ya waongofu wapya na mafunzo kwa washirika; kuanzisha na kuimarisha huduma za watoto, vijana na wanafunzi; kuanzisha na kutumia kwa utukufu wa Mungu vikundi vya sanaa na michezo; na kuanzisha na kutumia miradi inayoonesha upendo wa Yesu Kristo kwa jamii.

TUNAAMINI kwa uweza wa Mungu, kwa umoja na kwa pamoja, tutatenda **MAKUU** hadi kufikia malengo yafuatayo:

- **TUNAMWAMINI MUNGU KUWA NA UAMSHO** utakaomwagika nchi nzima na kusababisha mafuriko makubwa ya utendaji wa Roho Mtakatifu kwa kanisa kama matokeo ya kuinua viwango vya maombi yasiyokoma kwa mtu binafsi, makanisani, Sehemu, Jimbo, Idara ngazi zote na Taifa.

- **TUNAMWAMINI MUNGU KUWA NA UHAI NA UTENDAJI MPYA** katika kila kanisa kwa kufanya ibada zenye moto na maadhimisho ya Roho Mtakatifu katika ngazi ya familia, vikundi vidogo vidogo, makanisani na ngazi zote za kanisa.

- **TUNAMWAMINI MUNGU KUWA NA WASHIRIKA 9,000,000** ifikapo mwaka 2033. Hii ina maana kila mshirika ni mvunaji na hivyo anawajibika kuleta waongofu wapya wawili au zaidi kila mwaka.

- **TUNAMWAMINI MUNGU KUWA NA WACHUNGAJI 45,000** ifikapo mwaka 2033. Kila Mchungaji azae mchungaji mmoja au zaidi na kumwezesha kusoma chuo cha utumishi kila miaka mitatu.

- **TUNAMWAMINI MUNGU KUWA NA MAKANISA 40,000** ifikapo mwaka 2033. Kila miaka mitatu, kila kanisa lizae kanisa moja au zaidi na kulitegemeza.

- **TUNAMWAMINI MUNGU KUWA NA WAINJILISTI 4,000** ifikapo mwaka 2033 wanaohubiri katika upako na madhihirisho ya Roho Mtakatifu sawa na **Matendo 8:4-25.**

- **TUNAMWAMINI MUNGU KUWA NA WAMISHENARI 200 NJE YA NCHI NA KUFUNGUA MAKANISA 300** ifikapo mwaka2033. Kila jimbo liibue, lipeleke na kutegemeza wamishenari wasiopungua wawili (2).

- **TUNAMWAMINI MUNGU KUZIFIKIA JAMII 31** za makundi ya watu wasiofikiwa na injili ndani ya nchi kwa njia ya kupanda makanisa ifikapo mwaka 2033.

- **TUNAMWAMINI MUNGU** kuwa na elimu bora na imara na mafunzo kwa watumishi kwa kukamilisha mradi wa kila jimbo kuwa na chuo cha kupanda makanisa, kuendesha mafunzo endelevu, na kujenga na panua vyuo mama vya biblia kufikia udahili wa wanafunzi 3,000 kwa pamoja ifikapo mwaka 2033.

- **TUNAMWAMINI MUNGU** kuwa na vyombo vya habari vya kanda kama redio na TV na kuwa na chuo cha uandishi wa habari ifikapo mwaka 2033.

- **TUNAMWAMINI MUNGU** kuwa na ofisi mpya za makao makuu ya kanisa la nchi jijini Dodoma na kila jimbo kuwa na ofisi nzuri ya kisasa jimboni ifikapo mwaka 2033.

- **TUNAMWAMINI MUNGU** kuwa na miundo mbinu ya kisasa inayotumia teknolojia katika usimamizi wa rasilimali zake zikiwemo fedha, miliki na utawala ifikapo mwaka 2033.

- **TUNAMWAMINI MUNGU** kuwa na chuo kikuu kikubwa na bora katika fani mbalimbali, kila kanisa la mahali pamoja, jimbo na idara kuwa na shule ya chekechea, au msingi, au sekondari au vyote kwa pamoja na vituo vya afya ikiwa ni kutimiza wajibu wa kanisa kwa jamiii ifikapo mwaka 2033.

- **TUNAMWAMINI MUNGU** kufanya zaidi ya yale tunayoweza kuyafikiri na kuwaza kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu **(Waefeso 3:20-21).**

KWA KUTEKELEZA HAYO:

- Neno la Mungu ni Mwongozo wetu na mpango wetu wa kazi
- Kweli za Kibiblia zisizopotoshwa zitakuwa jumbe zetu za Injili
- Roho wa Mungu ndiye mwezeshaji na nguvu yetu ya huduma
- Damu ya Bwana Yesu Kristo inatuhakikishia ushindi
- Kanisa litakuwa na kuzidishwa kiroho, kiidadi, kijiografia, kiufanisi na kwa wana wapotevu kurudi kwa Bwana Yesu.

KAULI MBIU YETU

**"MIAKA KUMI NA TATU YA MOTO WA UAMSHO,
TUNAMTAKA BWANA NA NGUVU ZAKE**

**TUNAMTAKA BWANA NA NGUVU ZAKE,
MIAKA KUMI NA TATU YA MOTO WA UAMSHO**

**PAMOJA NA BWANA, KWA UMOJA NA KWA
PAMOJA, TUTATENDA MAKUU"**